

MATUMAINI PROG NO:2526

TITLE: WHERE ARE YOU?

SUMMARY: KINATUHIMIZA YA YA KWAMBA,MUNGU HUMJIA MTU KIBINAFSI.

TEXT: MWANZO 3:1-13

MADA: UKO WAPI?

.....

Hebu kwanza kabisa tukapate kuomba kabla ya kuendelea na somo hili la leo.
Natuombe;

OMBI.... Mfalme wa Wafalme,,Uliyetukuka juu ya vyote na yote; tunakushukuru kwa sababu ya ulinzi na zaidi mno uwepo wako. Tunapolianza somo hili la leo ,,tunakuomba ukatuongoze ili tukapate kulielewa vyema. Ni kwa Yesu tumeomba, Amina.

Mungu wetu ametujalia tena nafasi hii ambayo ni kujifunza kutoka Nenoni mwake. Ni tumaini langu kwamba unaendelea vyema kabisa. Karibu tuanze somo letu la leo lenye kichwa,,,*Uko wapi? hili ni swali ya kwamba,,Uko wapi?*
Kipindi hiki ni cha Matumaini kutoka TWR Kenya.
Somo ni kutoka kwenye Mwanzo 3:1-13.

Pale mwishoni mwa fundisho hili la leo,, nitakuwa na kupatia anwani yangu ya mawasiliano kati yetu.

Nataka kwanza kabisa ukabarikiwe kupitia kwa wimbo huu.....

WIMBO:

Ni kweli kabisa ya kwamba Baba yetu wa mbinguni alituumba tumwaabudu..Huyu akiwa ni Wonder Chibalonza Muliri **na wimbo Uliniumba Nikuabudu.**

Asante sana mtumishi Wonder kwa wimbo huo.....

Mimi naitwa, Vincent Amara.

Mpendwa,,sisi kama wanadamu bila ya kuwa na shaka yoyote wala maswali,,,sisi ni viumbe vya kipekee tena zaidi sana.

Sisi ni sehemu tofauti kabisa na zaidi sana ya kipekee katika ulimwengu wa viumbe ambavyo Mwenyezi Mungu Aliviumba.

Wale wanaoamini katika mageuzi ya viumbe au kwa kiingereza niseme (evolutionists), wanajaribu sana kutufanya tuamini ya kwamba sisi ni wanyama wa ngazi ya juu tu,,,tuliunganishwa na sokwe.

.....

Lakini Biblia inalo neno tofauti kabisa kwetu sisi.

Biblia inatuunganisha moja kwa moja na Mungu wetu. Maandiko yanatufundisha katika Mwanzo 1:26-27 kwamba;

"Mungu akasema, Na tumfanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu; wakatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani, na wanyama, na nchi yote pia, na kila kiumbe chenye kutambaa kitambaacho juu ya nchi. Mungu akaumba mtu kwa mfano wake mwenyewe, kwa mfano wa Mungu alimwumba; mwanamume na mwanamke aliwaumba."

.....

Msikilizaji wangu,,, neno hili halionyeshi hata kidogo kuwa sisi tumeunganishwa na sokwe! Sisi tumeunganishwa na Mungu aliyetuumba.

Msomi mmoja wa karne za nyuma kwa jina Franz Delitzsch, katika kitabu chake *A System of Biblical Psychology*, alifanya kazi kubwa sana ya kutafakari mstari wa Mwanzo 2:7 unaosema: "Bwana Mungu akamfanya mtu kwa mavumbi ya ardhi, akampulizia puani pumzi ya uhai; mtu akawa nafsi hai."

Anatufundisha kuwa mwili wa mwanadamu ulitengenezwa kwanza kabisa kabla ya nafsi,,, na ulitengenezwa kutoka kwenye ardhi ya Edeni ardhi ya furaha na utajiri ili mwanadamu awe kiungo kikuu kinachounganisha ulimwengu huu na historia ya kiungu, kabla ya Yehova-Elohim kupulizia pumzi ya uhai ndani yake. Bwana na Asifiwe sana, Amina!

Lakini ndugu mpendwa,,, matendo ya mwanadamu huyu wa kwanza yalisababisha swali kuu la kwanza kabisa kuulizwa na Bwana Mungu wakati Adamu alipokuwa amejificha kwenye miti.Mungu Aliuliza hivi,,Uko wapi? Swali hilo linapatikana katika Mwanzo 3:1-13, ambapo neno linasema:

1. Basi nyoka alikuwa mwerevu kuliko wanyama wote wa mwitu aliowafanya Bwana Mungu. Akamwambia mwanamke, Ati! Hivi ndivyo alivyosema Mungu, Msile matunda ya miti yote ya bustani?

² Mwanamke akamwambia nyoka, Matunda ya miti ya bustanini twaweza kula;

³ lakini matunda ya mti ulio katikati ya bustani Mungu amesema, Msiyale wala msiyaguse, msije mkafa.

⁴ Nyoka akamwambia mwanamke, Hakika hamtakufa,

⁵ kwa maana Mungu anajua ya kwamba siku mtakayokula matunda ya mti huo, mtafumbuliwa macho, nanyi mtakuwa kama Mungu, mkijua mema na mabaya.

⁶ Mwanamke alipoona ya kuwa ule mti wafaa kwa chakula, wapendeza macho, nao ni mti wa kutamanika kwa maarifa, basi alitwaa katika matunda yake akala, akampa na mumewe, naye akala.

⁷ Wakafumbuliwa macho wote wawili wakajijua kuwa wa uchi, wakashona majani ya mtini, wakajifanyia nguo.

⁸ Kisha wakasikia sauti ya Bwana Mungu, akitembea bustanini wakati wa jua kupunga; Adamu na mkewe wakajificha kati ya miti ya bustani, Bwana Mungu asiwaone.

⁹ Bwana Mungu akamwita Adamu, akamwambia, Uko wapi?

¹⁰ Akasema, Nalisikia sauti yako bustanini, nikaogopa kwa kuwa mimi ni uchi; nikajificha.

¹¹ Akasema, Ni nani aliyekuambia ya kuwa u uchi? Je! Umekula wewe matunda ya mti niliyokuagiza usiyale?

¹² Adamu akasema, Huyu mwanamke uliyenipa awe pamoja nami ndiye aliyenipa matunda ya mti huo, nikala.

¹³ Bwana Mungu akamwambia mwanamke, Nini hili ulilolifanya? Mwanamke akasema, Nyoka alinidanganya, nikala.

.....

Baada ya kulisoma neno hili,,,tunalizangatia haswa swali ambalo Mungu Alimuuliza Adamu ya kwamba,,, "Nani aliyekuambia ya kuwa u uchi? Je! Umekula wewe matunda ya mti niliyokuagiza usile?"

Kutokana na tukio hili na uzoefu huu,,, tunapata kuona sifa au misingi mitatu mikuu inayofanya utu na nafsi ya mwanadamu ili kutusaidia kuishi maisha ya kiwango cha juu.

Kipengele cha kwanza kabisa mtu wangu,,, ni kuhusiana na,,, Utu wa Kipekee wa Kila Mwanadamu yaani (*individuality*) kwa Kiingereza.

Dadangu,,,Swali ambalo Mungu aliliuliza lilikuwa linaelekezwa kwa Adamu moja kwa moja,,,kwamba,,*"Uko wapi?"*

Mzazi wetu wa kwanza Adamu alitambuliwa kama mtu binafsi mwenye uhusiano wa kipekee na Muumba wake.

Tukiirejelea historia,,,katika miaka ya 1960, kuna watu ambao walijaribu kujiundia kizazi chao wenyewe yaani ni "lazima iwe mimi",,, lakini walisahau kuwa huwezi kuwa "wewe" peke yako pasipo kuwa na watu wengine. Tofauti na Adamu aliyekuwa peke yake kama kichwa cha kizazi chote.

Mpendwa,,, sisi wa leo hii,,, tuko katikati ya wanadamu wengi.

Lakini nakuahidi ndugu pamoja na dadangu ya kwamba,,, Mungu anakujua wewe kibinafsi.

Haujapotelea kwa wengine mpendwa, kama ambavyo Adamu hakupotea katikati ya vichaka vya bustani! Alidhani anaweza kujificha lakini swali la Mungu lilimfanya asimame mbele zake. Mungu anakuja sasa hivi akikutafuta na kukuuliza, *"Uko wapi?"* Swali langu kwako ni je! wewe mwenyewe Utamjibu nini?

Kipengele cha pili, ni kuhusiana na,,, Uwajibikaji Wako Mbele za Mungu yaani (*Accountability*) kwa kiingereza. Mpendwa,,ule Uhuru ambao Adamu alipewa ili kufanya uamuzi wake wa kuwajibika,,,ulimfanya pia kumwaajibikia aliyempa uhuru huo. Katika Mwanzo 2:15-17, Mungu aliweka wazi mfumo huu wa uwajibikaji alipomwambia mtu kuwa anaweza kula matunda ya kila mti, bali mti wa ujuzi wa mema na mabaya asile, maana siku atakayokula atakufa hakika.

Ndugu yangu,,, kuwa na utu wa kipekee kunamaanisha kuwa na uwajibikaji. Kila uamuzi unaofanya,,bila shaka unabeba uwajibikaji ndani yake. Wakati Adamu na Hawa walipokula tunda walilokatazwa,,,walituletea matatizo matatu makubwa yanayotusumbua hadi wa leo.Yaani,,hatia, aibu, pamoja na Hofu.

Hatia iliwafanya wajifiche,,, aibu ikawafanya washone majani ya tini,,, na hofu ikawatawala. Hii inathibitisha wazi kwamba tunawajibika mbele za Mungu Muumba wetu!

Kipengele cha tatu na cha mwisho kwa leo kutokana na fungu hili,, kinahusiana na,, *Maisha ya Maadili na Maamuzi yaani (Morality)*.

Suala la maadili linadhihirika kupitia kwa maswali matatu ambayo Mungu aliyauliza baada ya Adamu kusema "Niliogopa... nikajificha". Mungu aliuliza: "*Nani aliyekuambia kuwa u uchi?*" kisha, "*Je, umekula matunda ya mti niliyokuagiza usile?*" na baada ya hapo akamwambia mwanamke, "*Ni jambo gani hili ulilolifanya?*"

Msikilizaji wangu,,uwajibikaji bila shaka unayazaa maadili. Sisi kama viumbe huru wenye uwezo wa kufanya maamuzi, kila uamuzi tunaoufanya unabeba matokeo ya kimaadili. Mungu alionyesha hili kwa kutaja adhabu na matokeo kwa nyoka, kwa mwanamke kupitia uchungu wa uzazi,, na kwa Adamu kupitia kula kwa jasho na kulaaniwa kwa ardhi. Maisha yameundwa na maamuzi yanayohusisha kupenda kwetu. Sisi ni viumbe wa maadili!

Rafiki yangu,,Mambo haya matatu yanashirikiana kwa pamoja kutuhimiza kuishi maisha ya kuwa wamakinifu sana. Utu wetu binafsi mbele za Mungu,, uwajibikaji wetu katika maamuzi tunayofanya,, na maadili yanayotutaka tusiwe upande usioeleweka yaani a (neutral position), maana kila tendo lina matokeo yake.

Sasa hivi ninakuuliza swali lile lile ambalo Mungu alimuuliza Adamu: "Uko wapi?" Nakuhimiza sana uweke uhusiano wako sawa na Mungu na kuyatafuta mapenzi Yake maishani mwako. Amen.

Ningependa kukutia moyo kwa kumalizia na lile neno letu kuu kutoka 1 Petro 2:9 linalosema: "Bali ninyi ni mzao mteule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu wa milki ya Mungu, mpate kuzitangaza fadhili zake yeye aliyewaita mtoke gizani mkaingie katika nuru yake ya ajabu."

Natumai ya kuwa,,umelipata fundisho zuri tena zaidi kupitia kwa somo hili la leo. Mungu na Akubarika sana,,Amina!

Ombi.....

Uliye tukuka Juu ya vyote na tena Mfalme wa wafalme,,tunakushukuru kwa ajili ya fundisho hili leo ya kwamba,,Uko wapi? Kwa kweli tutalizingatia kupitia kwa usaidizi wa Roho wako Mtakatifu.

Ni kwa Yesu tumeomba.....Amen.....

Rafiki yangu,,hiki Kimekuwa ni kipindi chako cha kujifunza neno Lake Mwenyezi Mungu. Kipindi cha matumaini kutoka Twr.Leo mada yetu imekuwa ni swali ya kwamba;Uko wapi?

Somo limetoka kwenye Mwanzo 3:1-13

Nitakuomba uwasiliane nami kupitia kwa anwani nitakayo kusomea mwishoni mwa kipindiki hiki cha leo. Anwani hiyo ni kwa ajili ya kusaidiana nawe.

Kabla yake,,u hapa wimbo There is power blood in the blood na Scripture

Harmonies,, ...

WIMBO.....

Na kwa kweli kabisa imo nguvu damuni mwa Yesu Asante sana waimbaji wetu.

ANDIKA BARUA AU UJUMBE WAKO UKIANZA NA NENO MATUMAINI TWR NA

KUTUMA KWA:

SLP 21514 CODE 00505

NAIROBI KENYA x2

Simu/Sms 0721970520 x2

Barua Pepe-barua@twr.co.ke

Kwenye Youtube ni @twr.co.ke

Mungu na akubarki sana Msikilizaji popote ulipo na,, hadi wakati mwingine, jina langu ni Vincent Amara.....Kwaheri